# MKATABA WA UTOAJI WA HUDUMA YA KUCHIMBA MITARO YA KULAZA MABOMBA YA MAJI KATIKA MRADI WA TAIFA WA KUPAMBANA NA MADHARA YA UGONJWA WA UVIKO KWA GHARAMA YA SHILINGI 1,100 KWA MITA

**KATI YA**

**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA KIGOMA**

Urban Water Supply and Sewerage Authority
KIGOMA / UJIJI

**NA**

**BAKARI JUMA S.L.P 44- KIGOMA**

**MEI 2022**

**MKATABA WA UTOAJI WA HUDUMA YA KUCHIMBA MITARO YA KULAZA MABOMBA YA MAJI KATIKA MRADI WA TAIFA WA KUPAMBANA NA MADHARA YA UGONJWA WA UVIKO KWA GHARAMA YA SHILINGI 1,100 KWA MITA.**

Makubaliano haya yamefanyika leo siku ya ..24..... Mwezi ....05......Mwaka 2022

**KATI YA**

**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA KIGOMA wa S.L.P 812** , KIGOMA(ambaye katika mkataba huu anajulikana kama "mwajiri au Mamlaka"neno ambalo linamjumlisha yeye mwenyewe na mrithi wa jina lake kisheria) kwa upande mmoja;

**NA**

**BAKARI JUMA** wa S.L.P 44 **KIGOMA** ambaye katika mkataba huu anajulikana kama "Mwajiriwa" neno ambalo linamjumlisha yeye mwenyewe na mrithi wa jina lake kisheria) kwa upande wa pili.

**KWAKUWA** Mamlaka ni taasisi ya umma inayoshughulikia na utoaji huduma ya usambazaji wa majisafi na usafi wa mazingira ndani ya manispaa ya Kigoma

**NA KWAKUWA** Mamlaka ni mmiliki halali wa kazi yote ya uchimbaji wa mitaro ya mabomba ya maji katika Manispaa ya Kigoma Ujiji.

**NA KWAKUWA BAKARI JUMA** ana uzoefu wakufanya kazi mbalimbali kama uchimbaji wa mitaro, ujenzi, utunzaji wa mazingira kwa ujumla.

**NA KWAKUWA** Mamlaka inadhamiria na nia kumwajiri BAKARI JUMA kutoa huduma ya kuchimba kwaajili ya kulaza mabomba ya maji katika Mradi wa taifa wa kupambana na madhara ya ugonjwa wa uviko ambapo katika mkataba huu itajulikana kama Mahali pa kazi;

**NA KWAKUWA** Mamlaka imeridhika na ubora wa kiutendaji kazi wa BAKARI JUMA katika kufanya kazi ya uchimbaji wa mitaro kwaajili ya kulaza mabomba ya maji.

***HIVYO BASI PANDE ZOTE KATIKA MKATABA HUU ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO;***

**1. WAJIBU WA BAKARI**

a) Kwamba, BAKARI JUMA atahakikisha kuwa anachimba mitaro hiyo kulingana na vigezo vilivyowekwa na Mamlaka yaani kina sentimita 80 na upana sentimita 40.
b) Kwamba, BAKARI JUMA atatakiwa kukamilisha kazi hiyo katika kipindi kisichozidi miezi mitatu (03)
c) Kwamba, BAKARI JUMA atatoa ushirikiano kwa uongozi wa Mamlaka juu ya maboresho yoyote yatakayotakiwa na pia atahusika na gharama zote kufanya matengenezo miundombinu ya maji iliyoharibiwa na mafundi wake'
d) Kwamba, BAKARI JUMA atatakiwa kuchimba na kufukia mtaro wa mita 39,000.

**2.0 WAJIBU WA MAMLAKA**

a) Kwamba, **Mamlaka** itamlipa BAKARI JUMA malipo yaliyokubalika ndani ya mkataba huu kwa mda uliokubalika kwa mujibu wa masharti ya mkataba huu.
b) Kwamba, **Mamlaka** itazingatia a kuheshimu masharti na makubaliano yalioainishwa ndani ya mkataba huu
c) Kwamba, **Mamlaka** itatoa ushirikiano kwa BAKARI JUMA katika kuboresha utendaji kazi pale itakapotakiwa.
d) Kwamba, **Mamlaka** itatakiwa kumlipa mwajiriwa Malipo yake yote pale atakapokamilisha kazi.
e) Kwamba, **Mamlaka** atamlipa Mwajiriwa kwa kuchimba mtaro mita 39,000 wenye upana wa sentimita 40 na kina chenye sentimita 80 ( kukatisha maeneo yenye barabara na hifadhi ya barabara kina ni mita 1.5) kwa TZS 1,100 kwa mita sawa na TZS 42,900,000/=

**3.0 MALIPO**

3.1 Kwamba, Mamlaka itamlipa BAKARI JUMA kiasi cha TZS 42,900,000/= kama malipo ya kazi yote kama ilivyokubaliwa kwenye mkataba huu kupitia benki yenye taarifa kama zitakavyowasilishwa na mwajiriwa.

3.2 kwamba malipo ya mkataba huu hayatabadilika isipokuwa kwa makubaliano ya maandishi ya pande zote mbili katika mkataba huu.

**4.0 MUDA WA MKATABA**

4.1 Kwamba, Mkataba huu utakuwa wa muda wa miezi mitatu (03) kuanzia tarehe ..24/05/2022 mpaka tarehe ....24/08/2022

**5.0 USITISHWAJI/UKOMO WA MKATABA**

5.1 kwamba, upande wowote wa mkataba utakuwa na haki ya kuvunja mkataba huu iwapo masharti ya mkataba huu yatakuwa yamekiukwa bila kuwepo na sababuzinazokubalika kisheria na upande wowote husika, kwa kutoa taarifa (notisi) ya siku 30 isiyo na malipo wala fidia.

**6.0 SHERIA ZINAZOTUMIKA**

6.1 kwamba makubaliano haya yatasimamiwa na sheria za mikataba za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

MAKUBARIANO haya yametiwa Saini na pande zote mbili na kushuhudiwa kwa nanma na tarehe iliyotajwa hapo awali kama ifuatavyo:

**KWA KUTHIBITISHA HAYO YOTE WAHUSIKA WAMETIA SAINI ZAO HAPA CHINI KAMA IFUATAVYO;**

Umetiwa chapa hapa **KIGOMA** na muhuri wa

**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA**

**MAZINGIRA KIGOMA**

hapa **KIGOMA**

leo tarehe ....24...... mwezi wa ....05.........2022

KIGOMA / UJIJI URBAN WATER SUPPLY AND SANITATION AUTHORITY P. O. Box 812 KIGOMA

.........................................

**MHURI WA MAMLAKA**

**UMESAINIWA NA/KWA NIABA YA MAMLAKA**

Saini..........................................................

Jina ....Mbike Amos Lyimo....................

Anuani ....S.L.P 812 Kigoma.....................

Wadhifa ....Mkurugenzi Mtendaji..................



Saini ...............................................................

Jina ... Fransisco Mafoye ...

Anuani ... S.L.P 812 ...

Wadhifa ... OSME. ...

Umetiwa chapa hapa **KIGOMA** na sahihi ya

**BAKARI JUMA**

hapa **KIGOMA** leo tarehe ...24... mwezi...05... 2022

..........................................

**SAHIHI YA BAKARI JUMA**

**UMESAINIWA NA BAKARI JUMA – KIGOMA**

Saini ...............................................................

Jina ... BAKARI JUMA ...

Anuani ... 0769443116 ...

Wadhifa ... FUNDI ...

Saini ...............................................................

Jina ... HASSAN RAMADHAN ...

Anuani ... 0755772312 ...

Wadhifa ... FUNDI ...